



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANA
OFISI YA RAIS,
TAWALA ZA MIKOZA ZA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA MANISPAA KAHAMA



Kumb.Na KMC/F20/19

30 Agosti, 2022

TANGAZO LA MIKOPO KWA WATUMISHI

Ofisi ya Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa Kahama imepokea barua kutoka kwa Katibu Mkuu Wizara ya Fedha na Mipango yenye Kumb.Na. EG.158/327/02'A'/443 ya tarehe 12 Agosti,2022 Iliyohusu taarifa ya mgao wa Fedha za utoaji Mkopo usio na Riba kwa Watumishi wa Umma kwa ajili ya kununua Magari /Pikipiki, Samani na Matengenezo ya Magari/Pikipiki

Kwa Tangazo hili Watumishi wote mnakaribishwa kutuma maombi kwa ajili ya Mkopo tajwa hapo juu chini ya masharti yafuatayo:-

- i. Mkopaji awe ni Mtumishi wa Umma wa Halmashauri ya Manispaa kahama.
- ii. Mkopo utazingatia kiwango kulingana na ngazi ya Mshahara na Mkopaji anatakiwa kubakiwa na 1/3 ya Mshahara wake baada ya Makato ambayo yatarejeshwa kwa kipindi kisichozidi Miezi 72.
- iii. Mkopaji atalipa Service charge (Gharama za kuandaa mkopo) 3% na protection Fund (Ulinzi wa Mkopo) 1% kutoka kwenye Mkopo huo.
- iv. Mkopaji anatakiwa kutuma barua ya maombi kwa Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Kahama.
- v. Barua ya maombi iambatanishwe na Nakala ya Hati ya Mshahara ya Mwezi Agosti, 2022.
- vi. **Mikopo hii hainunui deni kutoka Benki au Taasisi nyingine za Fedha.**

Maombi yote yatumwe kwa Mkurugenzi wa Manispaa Kahama na Mwisho wa Kutuma Maombi hayo ni tarehe 05/09/2022 saa nne Asubuhi.

Limetolewa:

C.B MKUSA

KAIMU MKURUGENZI
HALMASHAURI YA MANISPAA
KAHAMA



MUNICIPAL DIRECTOR
KAHAMA MUNICIPAL COUNCIL
OPT2
P.O. Box 472
KAHAMA